


**Issue no:** 01 | **Vol no:** 07 | **June** 2026: 35-50

# Ishara na Uashiriaji kama Mikakati ya Uchimuzi katika Riwaya za Maundu Mwingizi

**Neema George Mturo**

Tumaini University Makumira, Arusha, Tanzania.
Main author's email: neemamturo@yahoo.com

**Article History**
Received: **2026.03.17**
Accepted: **2026.04.19**
Published: **2026.06.08**

**Cite this article in APA**
Mturo, N. G. (2026). Ishara na Uashiriaji kama Mikakati ya Uchimuzi katika Riwaya za Maundu Mwingizi. *Editon consortium journal of Kiswahili*, *7*(1), 35-50. https://doi.org/10.51317/ecjkisw.v7i1.727

**Ikisiri**

Makala hii inachanganua ishara na uashiriaji kama mkakati wa uchimuzi katika riwaya za *Vita vya Mapenzi* (2012), *Mzimu wa Waufi* (2013), na *Tanzia* (2015) za Maundu Mwingizi. Tatizo lililochochea utafiti huu ni kuwepo kwa pengo la kitaaluma katika uchambuzi wa ishara na uashiriaji kama mkakati wa uchimuzi wa maudhui katika riwaya hizi. Hivyo, utafiti ulilenga kuchanganua matumizi ya ishara na uashiriaji katika kuchimuza maudhui mbalimbali. Makala hii imejikita katika nadharia ya Semiotiki iliyoasisiwa na Saussure (1916), ambapo ishara huundwa na kitaja (signifier) na kitajwa (signified), ambavyo vilitumika kama msingi wa uchambuzi wa data. Utafiti ulikuwa wa maktabani na ulitumia mkabala wa kimaelezo. Sampuli dhamirifu ilitumika kuteua riwaya teule, huku data zikichanganuliwa kwa mbinu ya uchanganuzi wa matini na matokeo kuwasilishwa kwa njia ya maelezo. Matokeo yalibaini kuwa mtunzi ametumia kwa ustadi ishara bia na zisizo bia, zikiwemo pete, rangi na mazingira, kuchimuza maudhui mbalimbali katika miktadha halisia na ya kihalisiajabu yenye matukio ya kutisha na kuogofya. Aidha, ilibainika kuwa ishara hizo zimeibuliwa kutoka katika visasili, historia na mitazamo ya kimaadili ili kuwasilisha ujumbe kuhusu masuala mbalimbali ya kijamii kwa kutumia mtindo wa uhalisiamazingaombwe. Utafiti unahitimisha kuwa ishara na uashiriaji ni mbinu muhimu za kisanaa zinazomwezesha Maundu Mwingizi kuchimuza maudhui kwa kina na kuchochea tafakuri kwa msomaji. Utafiti unapendekeza tafiti zaidi kuhusu matumizi ya ishara na uashiriaji katika kazi nyingine za fasihi ya Kiswahili kwa kutumia nadharia mbalimbali.

**Maneno Muhimu**: Ishara, kitaja, kitajwa, uashiriaji, uchimuzi.

Editon OPEN ACCESS

This article is distributed under the license of a Creative Commons Attribution-Non Commercial-ShareAlike 4.0 International License. It is permitted to be used, reproduced and distributed in line with Editon Consortium Publishing guidelines.

## UTANGULIZI

Katika taaluma ya fasihi, ishara na uashiriaji ni miongoni mwa mbinu muhimu zinazotumiwa kufichua maana zilizojengeka ndani ya matini, hususan zile zinazobeba ujumbe usiojitokeza moja kwa moja. Kwa mujibu wa Maguo na Alhabib (2020), Perrine (2014) na Chandler (2007), ishara hupanua upeo wa tafsiri kwa kumwezesha msomaji kufikia maana za kina zinazohusiana na mazingira ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni. Vilevile, Wamitila (2002) anabainisha kuwa matumizi ya ishara huongeza ubunifu wa kifasihi na kumpa msomaji nafasi ya kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa maana ya matini.

Katika fasihi ya Kiswahili ya kisasa, matumizi ya ishara yameendelea kuwa mbinu muhimu ya waandishi katika kuwasilisha maudhui nyeti na changamani bila kuyasema kwa uwazi. Kupitia ishara, waandishi huibua hoja zinazohusu uongozi, migogoro ya kijamii, maadili, mahusiano ya kijinsia, ukandamizaji, ushirikina na mabadiliko ya kijamii kwa namna inayomshawishi msomaji kufanya tafakuri ya kina. Hali hii imeifanya nadharia ya Semiotiki kuwa mojawapo ya lenzi muhimu za uchanganuzi wa kazi za fasihi kwa sababu huzingatia namna ishara zinavyozalisha maana katika miktadha mbalimbali ya kijamii na kitamaduni.

Riwaya za *Vita vya Mapenzi*, *Mzimu wa Waufi* na *Tanzia*, zilizoandikwa na Mwingizi, ni miongoni mwa kazi zinazodhihirisha matumizi makubwa ya ishara na uashiriaji. Riwaya hizi zinajengwa kwa matumizi ya matukio ya kinjozi, mazingira ya kutisha, wahusika wenye sifa za ajabu na visa vinavyoibua tafsiri mbalimbali za kifasihi. Aidha, riwaya hizi zinashughulikia masuala muhimu ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kimaadili yanayolikabili jamii ya sasa. Kutokana na sifa hizo, riwaya hizi zinafaa kuchunguzwa kwa kutumia nadharia ya Semiotiki ili kubainisha namna ishara mbalimbali zinavyounda maana na kuwasilisha ujumbe wa mwandishi.

Aidha, tafiti nyingi zimeelekeza nguvu katika maudhui, wahusika au mtindo, huku nafasi ya ishara kama mkakati wa kujenga maana katika riwaya hizi za kihalisiajabu ikibaki haijafafanuliwa kwa kina. Hivyo, bado kuna pengo la maarifa kuhusu namna ishara na uashiriaji vinavyotumika kujenga ujumbe na kuwasilisha dhamira katika *Vita vya Mapenzi*, *Mzimu wa Waufi* na *Tanzia*. Kutokana na pengo hilo, makala hii inalenga kuchunguza matumizi ya ishara na uashiriaji katika riwaya hizo tatu kwa kutumia nadharia ya Semiotiki. Utafiti huu unatarajiwa kuongeza maarifa katika uhakiki wa fasihi ya Kiswahili kwa kubainisha mchango wa ishara katika ujenzi wa maana, kuimarisha matumizi ya nadharia ya Semiotiki katika uchambuzi wa riwaya za Kiswahili na kutoa msingi wa tafiti zijazo kuhusu fasihi ya Kiswahili ya kisasa.

## MAPITIO YA MAANDISHI

### Ufafanuzi wa Dhana ya Ishara

Ishara ni kitu kinachosimamia kitu kingine kinachohusiana nacho. Kulingana na Frye na wenzake (1985: 451) “ishara ni kiashirii na kile inachosimamia ni kiashiriwa.” Kwa mfano, msalaba ni ishara ya Ukristo na rangi nyeusi kwa Wazungu ni ishara ya kuomboleza. Kwa maoni yao ishara huwakilisha kifikra maana na hali ya kitu kinachoashiriwa. Kwa mujibu wa Perrine (2014: 171) “ishara ya kifasihi ni kitu kilicho na maana zaidi ya kitu hicho. Yaani, ishara ni kitu, mtu, hali, tukio au kitu chochote kile kilicho na maana ya kawaida lakini kinaashiria au kinawakilisha maana nyingine zaidi.” Kutokana na maelezo haya ni wazi kuwa ishara si kitu pekee bali pia hurejelea tukio, hali au mtu anayeweza kutumiwa kudokeza maana kiishara. Kama anavyoongeza Snowden (2006: 85) ishara hujumlisha vitu hai na visohai pamoja na vitu dhahania. Kitu, hali au tukio linalotumiwa kiishara katika matini za kifasihi huwa na maana iliyo zaidi ya maana ya kawaida na inayohusiana na kiashirii.

Aidha, Eagleton (2018) anaeleza kuwa ishara katika kazi ya fasihi huwa sehemu ya mfumo wa kiitikadi wa jamii. Kwa mujibu wake, matini ya kifasihi haiwezi kutenganishwa na mazingira ya kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni yanayoizalisha. Hoja hii inaendana na matumizi ya ishara katika riwaya za Mwingizi ambapo ulimwengu wa majini, pete za kimiujiza na matukio ya kutisha yanatumika kuikosoa jamii inayotawaliwa na rushwa, usaliti, tamaa na unyonyaji wa kimfumo. Katika matini za kihalisia ishara huchukua sehemu muhimu na huwa dhahiri zaidi huhimili ujumbe na kuongeza maana. Riwaya zetu teule ni matini ambazo zinakiuka uhalisia kwa vile matukio mengi yamesimuliwa kupitia ndoto, uzungumzi wa nafsi ndani na mkondo wa ung’amuzi.

Katika matini nyingi za kifasihi ishara huweza kuwa na maana zaidi ya moja. Kutokana na mawazo ya Perrine, ishara ni kama kitu cha thamani chenye rangi nyingi kinachoweza kudhihirisha rangi mbalimbali kinapowekwa kwenye mwangaza (2014: 174). Maana

hizi za ishara hujitokeza kutegemea miktadha ya matumizi. Mawazo haya ya Perrine yanaungwa mkono na Meyer (2002: 179) anayedai kuwa maana za ishara zimekitwa katika mpangilio wa matini na kwa hivyo zinahimiliwa na miktadha ya matumizi yake. Miktadha hii inaweza kuwa ya kidini, kisiasa, kijamii au ya kiuchumi. Kwa mfano, DiYanni (1998: 509) anaeleza kuwa katika muktadha wa kawaida wa kijamii, maji ni ishara ya uhai lakini katika muktadha wa kidini maji yanayojitokeza kama mafuriko ni ishara ya kifo au majaribu. Kwa maana yake maji, yaani mafuriko ni ishara ya tukio baya. Katika muktadha wa kidini maji ni ishara ya uhai, usafi na tumaini. Ingawa ishara hutegemea muktadha fulani katika ufasiri wake, inaweza kueleweka kiyakinifu kwa kufahamu dhamira na muktadha wa kijumla wa matini. Kimsingi, ishara hailengi maana mahsusi bali hupendekeza maana inayohusiana na kiashirii.

**Ufafanuzi wa Dhana ya Uashiriaji**

Uashiriaji ni mbinu ya kifasihi ambayo ina historia ndefu. Kulingana na Abrahams (1971:170) uashiriaji kama mbinu ya kuwasilisha maana katika matini za kifasihi ilianzia kule Ufaransa katika karne ya 19. Abrahams anasema kuwa mwasisi wa mbinu hii alikuwa Baudelaire katika diwani yake ya mashairi Les Fleurs du Mal (1857), yaani "Maua ya Maovu." Aidha kadri siku zilivyosonga mbinu hii ikawa inatumika hata katika kazi nyingine za kifasihi ikiwemo riwaya kwani mwanzoni mwa karne ya ishirini Ulaya kazi nyingi za kifasihi zikiwemo mashairi, riwaya na michezo ya kuigiza zilidhihirisha matumizi ya uashiriaji, hususani zile zilizokuwa na mitazamo ya kidini na kijadi. Uashiriaji ulibainika katika matukio, mandhari na matumizi ya lugha.

Kwa mfano, katika riwaya ya Kusadikika (1951) ya Shaaban Robert mandhari ya nchi inayoelea angani inaweza kuangaliwa kama ishara ya taifa lisilo na msimamo wa haki, sheria na maendeleo thabiti. Nabukonde (2012: 5) akimnukuu T.S. Eliot, anasema kuwa "njia pekee ya mtu kuwasilisha hisia zake kwa umbo la sanaa ni kutafuta kitu au chombo chenye mahusiano kama vile mkusanyiko wa vitu, hali, mfuatano wa matukio, ambao utakuwa fomula ya kuwasilisha hisia hizo." Kutokana na maelezo ya Eliot uashiriaji ni mbinu muhimu katika kuwasilisha hisia za mtunzi na wahusika katika matini bila kuonekana kuibeza hadhira.

Perrine (2014: 173) anaeleza kuwa uashiriaji ni matumizi ya vitu au matukio katika kazi ya kifasihi kiishara. Mbali na vitu na matukio uashiriaji pia unahusu matumizi ya dhana, jina na mandhari kuibua maana za ziada akilini mwa msomaji. Nao akina Frye (1985: 452) wanadai kuwa uashiriaji ni matumizi ya kipekee ya ishara yanayodhihirisha neno kwa maana yake ya kawaida. Kwa mfano, neno waridi linarejelea ua linaloitwa waridi na dhana inayojitokeza nyuma ya maana, yaani urembo. Kwa sababu hii ua la waridi hutumika kuashiria urembo au umaridadi.

Uashiriaji hulenga kuibua maana mbili, maana ya kawaida ya kiashirii na maana inayohusishwa na kiashirii. Kama anavyodai Cirlot (1962: 14) uashiriaji kiyakinifu ni mfumo unaorejelea mahusiano changamano ambapo uhusiano mwimo ndio unaotawala. Uhusiano huu huunganisha hali halisi na hali dhahania. Hali halisi hurejelea maana ya kawaida inayojulikana na watumizi wa lugha husika ilhali hali dhahania hurejelea maana ya kifasihi inayowakilishwa na ishara. Kimsingi, uashiriaji ni mtindo wa kisanaa wa kutumia vitu, maneno, hali na tukio kwa kusudi la kuwasilisha wazo kidhahania.

Naye Meyer (2018) anaeleza kuwa ishara na uashiriaji katika kazi ya fasihi hujengwa kupitia marudio na msisitizo wa matukio ndani ya matini. Anasema kuwa ishara zinaporudiwa mara kwa mara hujenga dhamira kuu ya kazi husika. Katika riwaya za Mwingizi, matumizi ya mara kwa mara ya pete, damu, rangi nyekundu, giza na upepo yanasaidia kujenga dhamira za tamaa, maafa, mapambano ya kiroho, utawala wa siri na ukosefu wa maadili katika jamii.

**Ishara na Uashiriaji katika Kazi Mbalimbali za Fasihi**

Wanyonyi (2015) alichanganua ishara kama mbinu ya kimtindo ya kuwasilisha maana na kukuza uhusika katika riwaya ya Nyuso za Mwanamke (2010) ya Said Ahmed Mohamed. Lengo kuu la makala ya Wanyonyi ilikuwa ni kuchanganua na kubainisha jinsi ishara zinavyowasilisha maana na itikadi za jamii katika matini husika. Aidha katika utafiti aligundua katika riwaya hii ya *Nyuso ya mwanamke* kuna Ishara bia za jinsia ambazo zinazorejelea tofauti za kijinsia baina ya wanaume na wanawake. Kuna matumizi ya ishara inayorejelea mwezi ikimaanisha jinsia ya kike kwa sababu ina mpanuko. Pia kuna ishara za ndege na wanyama ambazo zimetumika katika matini kukuza maudhui ya utamaduni na itikadi za jamii.

Pia aliangalia ishara za nambari saba kama motifu inayojitokeza katika kazi nyingi za kifasihi hasa zenye mafungamano na Ukristo na Uislamu. Makala hii imetupa mwanga mkubwa katika uchambuzi wa makala yetu hasa katika kuilelezea vizuri ishara. Japo utafiti wa Wanyoji ulijikita zaidi katika ishara za maana na uhusika katika riwaya ya *Nyuso ya Mwanamke* na matokeo yalionyesha kwamba ishara hizi hizi zimebeba ujumbe wa mapenzi, itikadi na utamaduni, dhuluma dhidi ya wanawake wakati makala hii imejibana katika ishara na uashiriaji katika kuchumuza maudhui mbalimbali katika riwaya za *Vita vya Mapenzi*, *Mzimu wa Waufi* na *Tanzia*.

Wanazuoni Nabukonde na Perrine wanakubaliana uwepo wa ishara katika kazi za fasihi na mtunzi huzitumia kwa madhumuni mbalimbali. Nabukonde (2001) yeye anaona mtunzi anatumia ishara kuwasilisha hisi zake, zaidi anataja mahali ambapo vipengele vya kiishara huweza kutokea ambapo ni katika mkusanyiko wa vitu, hali na mfuatano wa matukio. Andiko lake limetusaidia kujua sababu ya mwingizi kutumia mbinu ya uashiriji ambayo huibua ishara na imetusaidia tunapochambua ishara katika kazi hii. Hata hivyo, mtazamo wake ni wa jumla, hataji ni aina gani ya sanaa moja kwa moja, kwani katika fasihi sanaa zipo nyingi.

Naye Perrine (2014.) andiko lake limetusaidia hasa anapoonyesha uashiriaji unaopelekea ishara kujitokeza katika kazi za fasihi na anataja vipengele ambavyo ishara hujitokeza mfano katika matumizi ya dhana, jina, na mandhari ili kuibua maana ya ziada kwa msomaji. Zaidi anaeleza katika kazi ya fasihi kuna matukio mengi ya kiishara. Pia amekuwa wazi na kuonyesha anazungumzia fasihi andishi kwani anaeleza ishara huibua maana za ziada kwa msomaji. Hata hivyo, hajaweka wazi ni utanzu gani katika fasihi andishi anauzungumzia hapa anatoa maelezo ya jumla akirejelea kazi za fasihi andishi. Utafiti wetu umetatua tatizo hili kwa kuchunguza ishara mbalimbali zilizojitokeza katika riwaya za Mwingizi.

**Msingi wa Kinadharia**

Makala hii imeongozwa na Nadharia ya Semiotiki iliyoasisiwa na Ferdinand de Saussure (1916), ambaye anaitazama lugha na mifumo mingine ya mawasiliano kama mfumo wa ishara. Kwa mujibu wa Saussure, kila ishara huundwa na vipengele viwili vinavyotegemeana, yaani kitaja na kitajwa. Kitaja ni umbo la nje la ishara linaloweza kuonekana, kusikika au kusomeka, ilhali kitajwa ni dhana au maana inayowakilishwa na umbo hilo. Saussure anasisitiza kuwa uhusiano kati ya kitaja na kitajwa si wa kiasili bali ni wa kimkataba na hutegemea muktadha wa kitamaduni na kijamii. Kwa sababu hiyo, ishara moja inaweza kubeba maana zaidi ya moja kulingana na mazingira ya matumizi yake.

Katika fasihi, nadharia ya Semiotiki hutumika kuchunguza namna watunzi wanavyotumia ishara kujenga maana ambazo haziishii kwenye maana za moja kwa moja bali huwasilisha ujumbe wa kina unaohitaji kufumbuliwa na msomaji. Kwa mtazamo huu, matukio, wahusika, vitu, rangi, mazingira na hata majina yanaweza kufanya kazi kama ishara zinazobeba maana za kisiasa, kijamii, kiuchumi na kimaadili. Hivyo, kazi ya mhakiki si kueleza maana ya juu juu ya ishara hizo pekee, bali kufafanua uhusiano uliopo kati ya kitaja na kitajwa pamoja na mchango wake katika kujenga dhamira za matini.

Mtazamo huu unaungwa mkono na Riffaterre (1978), ambaye anaeleza kuwa matini ya kifasihi hujengwa kwa tabaka la maana zilizo wazi na maana fiche. Kwa mujibu wake, maana halisi ya matini hupatikana kwa kuchunguza ishara zinazojirudia, miingiliano ya alama na muktadha wa matumizi yake. Hivyo, msomaji analazimika kuvuka maana za moja kwa moja ili kufikia ujumbe wa ndani unaokusudiwa na mtunzi. Hoja hii inaifanya nadharia ya Semiotiki kuwa nyenzo mwafaka ya kuchanganua riwaya teule zinazotumia kwa wingi lugha ya ishara na uashiriaji.

Aidha, Shemweta (2015) anaeleza kuwa nadharia ya Semiotiki inahusishwa kwa karibu na matumizi ya lugha ya ishara na uashiriaji, ambapo kitaja kimoja kinaweza kurejelea kitajwa kimoja au zaidi, au hata maana tofauti kabisa na ile ya kawaida. Kwa mfano, mtunzi anaweza kutumia kitaja "mbwa" kisirejelee mnyama halisi bali kikawa ishara ya kiongozi mbinafsi, dhalimu au mwenye tabia zisizokubalika katika jamii. Hivyo, maana ya ishara hutegemea muktadha wa matumizi yake badala ya maana yake ya kamusi.

Katika makala hii, nadharia ya Semiotiki imetumika kama mwongozo wa kubainisha na kufasiri ishara mbalimbali zilizojitokeza katika riwaya za *Vita vya Mapenzi* (2012), *Mzimu wa Waufi* (2013) na *Tanzia* (2015) za Maundu Mwingizi. Uchambuzi umejikita katika kubainisha kitaja kinachotumiwa na mtunzi, kitajwa kinachowakilishwa na ishara hiyo, pamoja na mchango wake katika kuchimuza maudhui ya riwaya husika. Kwa mfano, kitaja pete hakijatumika kuashiria

pambo la kawaida pekee, bali kimepewa maana mbalimbali kulingana na muktadha wa matini. Katika baadhi ya sehemu, pete ni ishara ya mikataba isiyo na usawa kati ya nchi zinazoendelea na nchi zilizoendelea, ambayo huchangia kuendeleza utegemezi wa kiuchumi na umaskini katika mataifa ya Dunia ya Tatu. Katika miktadha mingine, pete ni ishara ya viongozi wa dini wanafiki wanaotumia dini kama njia ya kujinufaisha kiuchumi badala ya kuwahudumia waumini.

Vilevile, ishara nyingine kama rangi, giza, upepo, kimbunga, mizimu na mazingira zimechunguzwa kwa kuzingatia uhusiano kati ya kitaja na kitajwa. Kwa mfano, giza halijachukuliwa kama ukosefu wa mwanga pekee bali kama ishara ya ukandamizaji, hofu, ujinga au kukosekana kwa haki; upepo na kimbunga ni ishara za misukosuko ya kijamii na kisiasa; ilhali mizimu na matukio ya kihalisiajabu yamefasiriwa kama mbinu za kisanaa zinazofichua migogoro, maovu na mivutano iliyopo katika jamii. Kupitia uchambuzi huu, nadharia ya Semiotiki imewezesha kufafanua jinsi Maundu Mwingizi anavyotumia ishara na uashiriaji kama mkakati wa kisanaa wa kujenga maana nyingi na kuchimuza maudhui yanayohusu siasa, uchumi, maadili na maisha ya jamii kwa ujumla.

**MBINU ZA UTAFITI**

Utafiti huu ulitumia mkabala wa kimaelezo na ulifanyika kwa kutumia mbinu ya utafiti wa maktabani. Mkabala huu uliteuliwa kwa kuwa uliwezesha kuchunguza na kutafsiri maana za ishara na uashiriaji zinazojitokeza katika matini za kifasihi kwa kuzingatia muktadha wake. Sampuli ziliteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji wa kimakusudi, ambapo riwaya za *Vita vya Mapenzi* (2012), *Mzimu wa Waufi* (2013) na *Tanzia* (2015) za Maundu Mwingizi zilichaguliwa kutokana na kubainika kuwa zimejaa matumizi ya ishara na uashiriaji, pamoja na kujengwa katika mtindo wa uhalisiamazingaombwe unaotegemea kwa kiasi kikubwa matumizi ya alama za kisanaa.

Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji wa matini. Mbinu hii ilihusisha usomaji wa kina na wa kurudiarudia wa riwaya teule ili kubaini vipengele vyote vilivyotumika kama ishara katika kujenga maudhui. Katika makala hii, ishara ilitambuliwa kwa kuzingatia vigezo vinne. Kigezo cha kwanza kilikuwa ni kujirudia kwa ishara katika sehemu mbalimbali za matini. Kigezo cha pili kilikuwa ni uwezo wa ishara kubeba maana inayozidi matumizi yake ya kawaida kwa mujibu wa Nadharia ya Semiotiki. Kigezo cha tatu kilihusu uhusiano wa ishara na dhamira kuu za riwaya, kama vile uongozi, dini, siasa, uchumi na maadili. Kigezo cha nne kilikuwa ni umuhimu wa ishara katika kusukuma mbele matukio au kufichua msimamo wa mtunzi kuhusu jamii. Kwa kutumia vigezo hivyo, ishara kama pete, rangi, na mazingira zilitambuliwa kama data za msingi za uchambuzi.

Baada ya ukusanyaji wa data, uchambuzi ulifanywa kwa kutumia uchambuzi wa maudhui wa kimaelezo. Mbinu hii ilichaguliwa kwa sababu ilimwezesha mtafiti kufasiri maana za ishara kwa kuzingatia muktadha wa matumizi yake badala ya kuhesabu idadi ya ishara zilizojitokeza. Uchambuzi uliongozwa na hatua za Willig (2001), ambapo hatua tatu zilionekana kufaa kutimiza lengo la makala hii. Hatua ya kwanza ilihusisha usomaji wa kina wa riwaya teule ili kupata uelewa wa jumla wa matini. Hatua ya pili ilihusisha kubainisha na kunukuu sehemu za matini zenye ishara na uashiriaji kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa. Ishara zilizobainishwa ziliainishwa katika makundi kulingana na aina na maana zake, kisha zikatafsiriwa kwa kutumia mihimili ya Nadharia ya Semiotiki, hususan dhana za kitaja na kitajwa. Hatua ya tatu ilihusisha kuhusianisha maana zilizopatikana na maudhui ya riwaya pamoja na kuwasilisha matokeo kwa njia ya maelezo yakifuatana na dondoo kutoka katika matini ili kuthibitisha hoja zilizojengwa.

Ili kuhakikisha uhalali wa data, ni ishara tu zilizojitokeza katika muktadha unaobeba maana ya kifasihi na zilizokuwa na uhusiano wa moja kwa moja na lengo la utafiti ndizo zilizojumuishwa katika uchambuzi. Aidha, tafsiri za ishara zilihakikiwa kwa kuzilinganisha na muktadha wa matini nzima, mihimili ya Nadharia ya Semiotiki, pamoja na maandiko ya wataalamu mbalimbali kuhusu ishara na uashiriaji katika fasihi. Utaratibu huu ulihakikisha kuwa tafsiri zilizotolewa zilikuwa na msingi wa kinadharia na kimuktadha. Kwa upande wa uaminifu wa utafiti, ulizingatiwa kwa kutumia utaratibu uleule wa ukusanyaji na uchambuzi wa data katika riwaya zote tatu. Vilevile, vigezo vilevile vya utambuzi wa ishara vilitumika katika matini zote, huku kila tafsiri ikiungwa mkono na dondoo husika kutoka katika riwaya zilizochunguzwa.

## MATOKEO YA UTAFITI

### Mbinu za Kiishara na Uashiriaji jinsi Zilivyochimuzwa katika Riwaya za Maundu

Mwingizi ametumia ishara nyingi sana katika riwaya zake, lakini katika makala hii tumeweza kujadili ishara chache tu, ambazo ni ishara ya pete, ishara ya maumbile asilia (mazingira) na ishara za rangi mbalimbali alizozitumia. Riwaya teule za Maundu Mwingizi zinampa msomaji uwanja mpana wa kuzitafsiri ishara kwa mujibu wa lugha aliyoitumia mwandishi na upana wa mawazo yake. Usimulizi wake umejaa ishara na uashiriaji ulioibuliwa kutoka katika visaasili, historia na mitazamo ya kimaadili. Zifuatazo ni ishara ambazo tumezijadili katika riwaya hizi kwa kifupi: -

### Pete kama Ishara na Uashiriaji

Pete ni ishara ya ahadi, maamuzi, kumbukumbu, mtindo, na mara nyingine ndoa, na maana yake hubadilika kuling ana na kidole unachovaa BAKITA (2023). Aidha tunaweza sema pete ni kitu cha duara ambacho kimekuwa kikivaliwa na watu wengi duniani katika vidole vya mikononi, baadhi ya watu wamekuwa wakivaa pete kama pambo tu, na wengi wao wakivaa pete kama naziri fulani au wamewekeana mkataba juu ya kitu fulani kama vile uaminifu, heshima na mapenzi miongoni mwa wanandoa, na baadhi ya viongozi wa dini.

Uvaaji pete kwa wengine ni utii wa kaida za kitamaduni, utekelezaji au utimishaji wa miiko fulani, kwa wengine pete ni ufunge wa uanachama wa kundi au shirika, na wapo wengine ambao kwao pete ni mikataba ya kiuganga na uchawi. Kwa jumla pete ni kitu kilicho na historia ndefu na matumizi na maana pana. Lakini katika miktadha ya kifasihi pete imekuwa ikitumika kama ishara ya kiuradidi kama asemavyo Birkerts (1993: 113) kuwa ishara za kifasihi hupata maana kwa kutumiwa kiuradidi katika kazi ya kifasihi au kwa kuwekwa kimakusudi kisanaa katika tukio. Ndiposa tunaona kazi nyingi za fasihi zimesheheni ishara ambazo zimetumiwa kiuradidi kiasi kwamba husaidia kusisitiza ujumbe na vile vile hufanya kazi kama vikale (Wa Mutiso1996: 19-20).

### Pete kama Ishara Inayoashiria Ulinzi, Utajiri, Ulaghai, Mikataba Hewa, Unyonyaji

Katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi* pete anayovishwa Suhail ni pete ya *Khatam Budha* ambayo ni ishara ya ulinzi na utajiri. Pete hiyo inabadilika rangi kutokana na muktadha na matukio yanayomzungukia mvaaji. Pete ina masharti ya kunyeshwa damu ya kila mwezi. "Naam ni damu ya mbuzi, sasa vua pete yako kisha uiweke humo ndani ya bakuli (uk. 66)." Pete hiyo inatumika kama ishara maradufu ya maangamizo na neema. Inajenga maudhui ya kuwaangamiza watu wabaya, wasaliti na waongo. Mtu anapolazimika au kulazimishwa kuivaa ni sawa na kuhakikisha kuwa anaendeleza matakwa ya waliomvisha au walioingia nao mkataba. Hakuna nafasi ya kuisaliti. Ni ishara ya kufungwa, kudhibitiwa kihali na kimawazo, kutawaliwa kifikra na kiutendaji, yaani kubanwa kwa uhuru wa kufikiri na kutenda, kuondolewa na pengine kudhibitiwa kwa hiari ya mtu binafsi kutenda.

Kwa mfano, Suhail anapojitokeza katika hali zake mbalimbali za kiutendaji, hapana shaka kwamba Suhail ni chombo tu, hakuna alitendalo kwa kuamua kwa njia razini ila kwa kuelekezwa, kutishwa au kushawishiwa. Anatawaliwa katika kila hali na hata anapotumia uongo na ulaghai, ni kwa sababu ya kuogopa matokeo yaliyo kinyume na matakwa ya waliomvisha pete au kukiuka masharti ya hao hao waliomvisha pete. Baudrillard (1998) anaeleza kuwa vitu vya alama katika jamii ya kisasa huwa na nguvu ya kudhibiti fikra na matendo ya binadamu. Kwa mujibu wake, alama kama pete zinaweza kuwa nyenzo za mamlaka fiche zinazomfanya mhusika aishi ndani ya mfumo wa udhibiti bila kujitambua.

Vilevile pete hiyo inaashiria kielelezo cha ulaghai, mikataba hewa, na kufungamanishwa na matajiri na walio na uwezo. Suhail anaingizwa katika vita ambayo si yake anashirikishwa na kuathirika katika vita ya kitabaka, vita ya binadamu na majini, vita ya majini kwa majini, vita ya kijinsia yakizingatiwa mahusiko yake katika mahusiano na Shekhia na Sharifa, vita ya kifamilia, vita ya kiutambuzi, vita vya kitaifa, vita vya kiuzao, vita ambapo mahusiko yake ni kama chombo tu. Kila anapotumia nguvu zake kujinasua katika mitego mbalimbali, mafanikio yake ni duni sana au hata hakuna mafanikio, kwa mfano alipougua ugonjwa usiojulikana hatima yake ni kaburi tu.

Suhail amevishwa pete ya kijani aliyokuwa akiitumia kama video ya kuyaangalia mambo yaliyokuwa mbali yaliyokuwa ya hatari na misukosuko.

> *Suhail alipoipokea tu akaivaa kidoleni kama vile anayeijaribisha kisha akakibenjua kitufe kidogo sana kilichopo kwa upande wa nyuma wa kile kito cha rangi nyekundu ili aweze kuona*

> *ni hatari gani inayomnyemelea (uk. 211).*

Hivyo basi pete imeashiria kama zana ya ulinzi na kiona mbali cha miujiza. Kuvikwa pete ni ishara ya kukabidhiwa madaraka ya kiutawala na umiliki wa rasilimali, lakini kama chombo tu kwa sababu mali na rasilimali hizo zinadhibitiwa kwa njia fiche na wamiliki wenyewe. Ni alama ya uongozi wa umma kwa maana ya kutumikishwa na kuoneshwa ilhali waongozao ni wengine. Kwa upande mwingine, Chul Han (2017) anasema kuwa mifumo ya kisasa ya utawala hutumia ishara na mikataba fiche kuwafanya watu wajikabidhi wenyewe katika mifumo ya utumwa mpya. Hoja hii inaonekana katika uhusiano wa Suhail na pete ya Khatam Budha ambapo anajikuta akiingia katika vita visivyo vyake; vita vya majini, vita vya kifamilia na migogoro ya kijamii.

Pete inamfanya kuwa mtumishi wa nguvu kubwa zinazodhibiti maisha yake kwa siri. Hivyo, pete ni ishara ya ukoloni mamboleo unaowafanya watu na mataifa kuingia mikataba inayowanyonya. Aidha, Ngũgĩ wa Thiong'o (2021) anaeleza kuwa fasihi ya Kiafrika hutumia ishara mbalimbali kufichua namna mataifa ya Afrika yanavyofungwa na mikataba ya kiuchumi na kisiasa inayowanufaisha wakoloni wapya. Hoja hii inaonekana pale Suhail anapolazimika kutekeleza masharti ya pete hata yanapomletea migogoro katika familia na jamii. Pete inaashiria mikataba ya kimataifa inayowafanya viongozi wa Afrika washindwe kusimamia maslahi ya wananchi wao.

Ishara ya pete inaonekana tena katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi* ambapo Masumbuko aliye mwanaume anayeoteshwa kufanywa mwanamke aitwaye Shamsa na kupangiwa kuolewa na mwanaume chini ya usimamizi wa Hunudu kama sehemu ya adhabu ya kukataa kujiunga na himaya ya Waufi. Baada ya kuonyesha dalili za kukubaliana, Hunudu anamvisha pete Masumbuko, mtunzi anasema: -

> *Katika kidole cha kati, mara ghafla akaanza kubadilika na kurudi katika maumbile yake ya awali, lakini ghafla akaanza kujisikia vibaya mwili mzima…kama mtu anayekaribia kukata roho (uk. 75).*

Pete anayovikwa Masumbuko katika *Mzimu wa Waufi* ni pete ya kijini na inatumika kumtibu na kumrudishia hali yake ya kijinsia. Kama ambavyo Shekhia alivyotumia pete yake kumponyesha Sharifa katika *Vita vya Mapenzi*, ndivyo jini Hunudu alivyofanya. Pete hiyo aliyovikwa ndotoni anakuja kujikuta akiwa nayo *"mkononi katika kidole chake cha kati cha mkono wa kulia (uk. 77 Mzimu wa Waufi)."* Pete hiyo haionekani kwa watu wa kawaida. Kila aliyeingizwa katika kundi la Waufi alikuwa na *"pete kubwa nyekundu"* akiwemo Sheikh Mwinyigoha. Ishara ya pete katika riwaya za *Vita vya Mapenzi* na *Mzimu wa Waufi* zinakitwa katika kubainisha mambo mengi mseto; mkataba kati mvaaji na aliyemvalisha kama vile kundi la majini au mitandao ya siri, utawala, udhibitiwaji na uelekezwaji, utumikishwaji na ufiche wa mambo mengi hasa yale yasiyo halali.

Katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi* tunaona ukutanaji wa Suhail na Sufian ulikuwa katika mazingira sadfa kwa Suhail lakini kwa upande Sufian alikwishakuyajua mazingira ya kukutana kwake na Suhail kwa kutumia nguvu zake za kimajini. Kwa hiyo wanakutana katika gari na gari linapata ajali pasipo Suhail kuelewa chochote kinachoendelea kwani abiria mbalimbali waliokuwepo katika ajali wanakufa. Mzee huyu anakuwa katika hali mbaya na Suhail anatoka mzima, lakini mzee huyu anajitahidi kuhakikisha anamkabidhi pete na pesa katika mazingira ambayo si ya kawaida, mazingira ya kutisha na kuogofya, mazingira ya umwagikaji damu na ufu.

Mtunzi anaonyesha kwamba hii inaashiria kwamba mikataba inayoasisiwa na kuibuka katika hali kama hizi ni mikataba hatari itakayosababisha umwagikaji wa damu na vifo. Si ajabu huo ndio uliokuwa uhalisi wa maisha ya Suhail. Ni kitu cha ajabu sana kufanya mikataba kama hiyo katika mazingira na miktadha ya ajali, hasa ajali ambapo kuna umwagikaji wa damu na vifo vya watu. Lakini pamoja na kumkabidhi pete hiyo, mtunzi anaonyesha kuna masharti ambayo amepewa na ahakikishe anayatekeleza masharti hayo. Kwa mfano, katika uk. 9 mtunzi anasema:-

> *Mzee Sufian akavua pete yake kubwa yenye kito cha rangi ya njano aliyokuwa ameivaa kwenye kidole chake na kumshika Suhail mkono, kisha akamvalisha (uk. 9).*

Mtunzi anatuonyesha kwamba kile kitendo cha kumvalisha Suhail pete na kumpa masharti mbalimbali

kilikuwa kinashiria makubaliano mazito kati ya Sufian na Suhail bila yeye mwenyewe Suhail kujua kwamba hayo makubaliano ya pete na masharti yatakuja kumuangamiza. Aidha mtunzi anaonyesha uvukaji wa mipaka katika hayo makubaliano kwani Suhail ni mwafrika na mzee Sufian yeye ni muasia anatoka nchini Yemen wanakutana katika mazingira tatanishi na siku hiyo hiyo wanaingia katika makubaliano. Hivyo basi mtunzi kupitia ishara hii ya pete anachimuza dhamira ya unyonyaji kwani pete huvaliwa na watu wenye mikataba fulani fulani. Naye Mbembe (2019) anaeleza kuwa mifumo ya kisasa ya mamlaka hujengwa kupitia mikataba inayowafanya watu waishi katika hofu na utegemezi wa kudumu. Katika riwaya za Mwingizi, pete inakuwa alama ya mamlaka ya siri yanayowatawala wahusika. Suhail hawezi kuvunja masharti ya pete bila kupata madhara. Hii inaashiria namna mifumo ya kisiasa na kiuchumi inavyowafanya wananchi na viongozi wa mataifa maskini kuendelea kuwa watumwa wa mikataba yenye manufaa kwa mataifa yenye nguvu.

Kwa upande mwingine mtunzi ametumia pete kama ishara ya kuonyesha kwamba Suhail na mzee Sufian wamekubaliana mpaka kufa katika kutimiza masharti aliyompa ndio maana akaamua kumvalisha pete ya kuonyesha ishara ya makubaliano yasiyovunjika. Mwandishi kupitia pete anaashiria wazi jinsi mataifa yaliyoendelea yanavyotumia njia mbalimbali katika kuhakikisha wanaingia mikataba na mataifa yanayoendelea ili waweze kuzinyonya nchi hizi, kwani pete inaonyesha ni makubaliano na masharti wanayoyatoa nchi ambazo zimeendelea kwa nchi zinazoendelea katika kuhakikisha mikataba yao haivunjiki.

Aidha mtunzi anaonyesha wazi kabisa njia mbalimbali wanazozitumia katika unyonyaji huu ni kutengeneza mazingira na kuhahakisha wanazubaisha waafrika kwa kutumia mbinu mbalimbali za kuwaangamiza kifikra ili wasiweze kuhoji viongozi wao mambo mbalimbali yanayoendelea kwa kuwapumbaza. Ndio maana ile ajali ya wale abiria waliokuwepo kwenye gari na wakapata ajali na kuuwawa lakini Suhail anapona na Sufian anakufa ni ishara ya kuwaangamiza mataifa ya ulimwengu wa tatu kifikra ili waendelee kudumaa na wenyewe wakiendelea kuchota mali asili zetu. Kama alivyosema Walter Rodney (2014) kuwa mataifa ya Afrika yameendelea kunyonywa rasilimali zake na mataifa yaliyoendelea kupitia mifumo mbalimbali ya kiuchumi na kisiasa.

**Pete kama Ishara Inayoashiria Ukombozi, Uendelezaji na Uimarishaji wa Maslahi Binafsi**

Kwa upande mwingine mtunzi anaonyesha pete ya Suhail aliyopewa na mzee Sufian hubadilika rangi kutokana na matukio kuna wakati wakiwa wanafuatiliwa na maadui zao yaani serikali ya himaya ya Budha huwa na rangi nyekundu na wakati kuna amani pete ile huwa inakuwa na rangi ya njano. Mtunzi ametumia pete kama ishara ya ukombozi ambayo huwaweka tayari mzee Sufian na majini wa himaya ya Budha kupambana pale wanapofuatiliwa katika mipango yao. Mtunzi kupitia pete hii anachimuza dhamira za ukombozi kwani pete hii ilikuwa ikitumiwa na akina Sufian kwa ajili ya kujikomboa na mahasimu wao.

Aidha mwandishi ametumia tena pete kama ishara ya kuchimuza maudhui mbalimbali kama vile uendelezaji na uimarishaji wa maslahi binafsi, uwepo wa mitandao siri lakini inayokwenda sambamba na mitandao rasmi ya kijamii. Katika uk. 52 mwandishi anaonyesha pete ndio chanzo kikubwa cha uchumi katika himaya ya Budha, jambo ambalo kwa kuwa ni la kimajini, linaweza kukubalika. Kwani pete ndio iliyokuwa ikibeba uchumi wa himaya ya Budha na watu walikuwa wanagombana kwa ajili ya maslahi yao binafsi kila mtu anataka kujineemesha yeye mwenyewe kutokana na uchumi mkubwa uliopo kupitia hiyo pete.

**Pete Imetumika kama Ishara Inayoashiria Usaliti, Kuleta Migogoro na Kutatua Matatizo**

Vilevile pete imetumika kama ishara ya usaliti na kuleta migogoro katika familia kwani sababu ya Suhail kumuacha mchumba wake ni kutokana na makubaliano ya pete ambayo alipewa na Sufian. *Vita vya Mapenzi* uk 70 …. Miongoni mwa masharti aliyopewa kuhusiana na ile pete ilikuwa ni kumuoa Shekhia na kumuacha mchumba wake wa zamani Sharifa…. Pete ile iliweza kuleta pia mgogoro mkubwa sana kati ya Suhail na wazazi wake pindi walipomtaka amuoe mchumba wake wa siku nyingi. Aidha ndoa hii inakuwa ngumu kwa ajili ya mkataba wa pete ndivyo mataifa yanaendelea pia viongozi wake wanakuwa na migogoro mikubwa sana na wakati mgumu kwa wananchi wao kutokana na masharti ya mikataba waliyopewa na wawekezaji pamoja na mataifa yaliyoendelea yanayotoa misaada kwa nchi maskini.

Mtunzi anatumia pete kama kitu ambacho kina uwezo mkubwa wa kimaajabu katika kutatua matatizo mbalimbali, kwani pete imetumika kumwokoa Sufian

kutoka katika mikono ya mahasimu wake huko nchini Yemen (*Vita vya Mapenz*i uk 170). Mtunzi anaonyesha kwamba pindi Sufian alipokuwa anapigwa na mahasimu wake pete ile aliyokuwa ameivaa Suhail iliweza kuwaka rangi nyekundu ikiashiria kuna matatizo makubwa yametokea kwa mzee Sufian. Ndipo Suhail akaitumia ile pete kufika mpaka nchini Yemen kwa dakika kumi na tano tu. Mtunzi kupitia ishara hii ya pete anachimuza ujumbe wa jinsi ambavyo viongozi wengi au hata watu maarufu hutumia nguvu za kichawi na kishirikana katika kujikinga na mahasimu wao au katika kuzilinda nafasi zao ili waendelee kubaki mamlakani.

**Pete Imetumika kama Ishara Inayoashiria Uchimvi na Kinga**

Aidha katika riwaya hii ya *Vita vya Mapenzi* uk wa 95, *pete* imetumika kama ishara ya uchimvi kwani imekuwa ikiashiria majanga mbalimbali ambayo yatatokea mbele. Uchimvi ni hali ya kutoa tahadhari au kufichua njama na hatari zitakazomkabili mhusika, ambapo ishara hutumika kubainisha uwepo wa tishio au matokeo mabaya yanayoweza kutokea BAKITA (2023). Mfano mzuri ni Suhail alipofanya mapenzi na Sharifa pete ya Shekhia iliwaka moto ikiashiria kuna ukiukwaji wa makubaliano ya masharti aliyopewa Suhail na Sufian pamoja na mwanaye Shekhia, hivyo pete ilikuwa ni kama kitu cha tahadhari. Mfano mwingine ni pindi Suhail alipoongea uongo kwa mzee Atrash pete ile iliweza kumuonyesha rangi nyekundu kwa kuonyesha kwamba kitu anachokifanya si kizuri na mwisho wa siku kitamletea matatizo. Uashiriaji wa matukio ya mbele ya pete hii umechimuza dhamira ya uwongo kwa watu kuachana na uongo kwani mwisho wa uongo huwa si mzuri kama ambavyo imemtokea Suhail mpaka akafa sababu kubwa ni uongo.

Katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi* pete imeashiria kama ni kinga. Mtunzi anamuonyesha Masumbuko akibadilika kutoka ile hali ya uanaume na kuwa mwanamke baada kuvalishwa pete na jini Hunudu katika uk. 75 katika kuashiria kwamba pete kama kinga na chombo ambacho kinawasaidia watu kutoka katika hali ngumu ya maisha au matatizo mbalimbali. Mtunzi kupitia ishara ya pete anachimuza dhamira ya kinga mbalimbali ambazo watu hujiwekea katika biashara zao au maofisini mwao ili waendelee na wasisumbuliwe na mahasidi wao. Mtunzi anaendelea kutumia ishara ya pete kama chombo ambacho hutumika na viongozi wengi serikalini katika kuzitetea nafasi zao. Aidha wafuasi wote wa Hunudu walikuwa wana pete na kama kuna kitu cha hatari mbele yao pete ilikuwa inaonyesha miale ya rangi nyekundu ili waweze kujikinga. Mtunzi anaonyesha jinsi viongozi wengi serikalini hutumia uchawi na ushirikina kama kinga ya kuzitetea nafasi zao. Kwa hivyo, katika hali hizi, pete ni kitu sawia na mtandao wa kimahusiano yawayo yoyote yale, yawe na tija au yawe na shari. Ikumbukwe kwa umbo la pete ni umbo duara, na mduara unaibua imani za aina nyingi katika jamii mbalimbali.

**Pete kama Ishara Inayoashiria Chombo cha Maslahi Binafsi na Migongano ya Kidini**

Mtunzi bado anaendelea kuchimuza dhamira ya maslahi binafsi na migongano ya kidini kupitia riwaya ya *Mzimu wa Waufi*. Pete iliweza kuleta migongano mikubwa katika jamii katika suala la dini, kwani pindi alipoitwa mchungaji amwombee Masumbuko, majini aliyokuwa nao, yule mchungaji naye alionekana amevaa pete hiyo hiyo ya kimajini aliyovalishwa Masumbuko na Hunudu. Watu wote walikuwa hawaioni hata baba yake Masumbuko isipokuwa Masumbuko tu ndio alikuwa anaiona. Pia sheikh mwingine alipoitwa kumsomea kisomo kule hospitalini alionekana amevaa pete hiyo hiyo ya kimajini. Mtunzi anaonyesha jinsi ambavyo hata viongozi wengi wa dini huwa kinyume na dini na wapo katika dini kwa ajili ya maslahi yao binafsi. Tazama dondoo ifutayo katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi* imedhihirisha haya;

> *Wewe Masumbuko una matatizo gani Huyu mzee hafai kuwa Sheikh huyu, nawaeleza si Sheikh huyu, naye ni mfuasi wa Waufi! Mnaona pete yake hiyo na hii yangu waliyonivisha inavyofanana? (uk. 79)*

Mwandishi anamuonyesha Masumbuko anawashangaa viongozi hawa wa dini wanaotumia pete kama ishara ya kufanya mambo ambayo ni kinyume na dini zao. Mtunzi kupitia ishara hii ya pete anaonyesha jinsi viongozi wengi wa dini jinsi walivyo wanafiki nje wanafanana na kondoo kumbe ndani ni mbwa mwitu. Baadhi ya viongozi wa dini wamekuwa wakitumia dini na vyeo vyao katika kujitafutia mali kwa njia mbalimbali zisizo halali. Kwa mujibu wa Mbiti (2022) anasema vitu vya kiibada na alama za kimila kama pete katika jamii nyingi za Kiafrika huhusishwa na nguvu za kiroho, kinga na utambulisho wa kijamii. Aidha mtunzi anatumia pete kama ishara ya udhibiti wa kiuchumi na ishara ya udhibiti wa maslahi ya kibinafsi kwa kuonyesha viongozi hawa wa dini jinsi wanavyofanya maovu yao mbalimbali

na wanatumia mgongo wa dini ili watu waweze kuwaamini na waweze kukubalika katika kuhakikisha wanaendelea kudhibiti uchumi wao. Aidha Mulugu (2016) anadhihirisha kwa kuonyesha jinsi ambavyo viongozi wengi wa dini walivyoleta migongano katika jamii na wako kwa ajili ya maslahi yao binafsi si kwa ajili kuwasaidia zaidi waumini wao.

Kwa mintarafu hii pete imetumika mara kwa mara katika riwaya hizi teule katika kubeba ishara nyingi sana zenye jumbe mbalimbali kwa upande mwingine. Harari (2015) anasema kuwa jamii nyingi hujengwa juu ya “hadithi za pamoja” na alama zinazowafanya watu kuamini katika mifumo fulani ya mamlaka. Pete katika *Vita vya Mapenzi* na *Mzimu wa Waufi* inakuwa alama ya kuaminika kwa mfumo wa Khatam Budha na Waufi. Wale wanaovishwa pete wanakuwa sehemu ya kundi maalumu lenye siri, mamlaka na masharti yake. Hivyo pete ni ishara ya uanachama wa nguvu za siri zinazotawala jamii.

**Rangi kama Ishara na Uashiriaji**

Kwa mujibu wa Turner (1967), rangi katika jamii nyingi huwa na maana za kiutamaduni zinazohusiana na maisha, kifo, nguvu na mamlaka. Katika riwaya hizi, rangi nyekundu inawakilisha nguvu za giza na umwagikaji wa damu unaotokana na tamaa ya mali na madaraka. Tunapozungumzia ishara za rangi kupitia kazi teule za Maundu Mwingizi tunajikita na rangi nyekundu, nyeusi, kijani, nyeupe na njano zikichimuzwa kwa wingi kuashiria mambo mbalimbali ikiwemo ishara za kifo, uponaji, utakaso, hali ya kawaida, ubaya au ulozi. Macho ya wasomaji yanapelekewa kuangazia rangi mbalimbali zinazochimuzwa kwa wingi zikiwa zinalenga kuashiria masuala mbalimbali.

Begi jekundu la pesa katika *Vita vya Mapenzi* linakabidhiwa kwa Suhail na kiumbe jini-mtu, Mzee Sufian wakati akiwa katika dakika za kukata roho akizungukwa na damu nyingi. Kwa mujibu wa Leeuwen (2016), rangi katika maandishi ya kifasihi na kisanaa huwa ni mfumo wa mawasiliano unaobeba maana za kijamii na kiitikadi. Leeuwen anaeleza kuwa rangi nyekundu mara nyingi huhusishwa na hatari, vurugu, nguvu na tahadhari. Mtazamo huu unaonekana wazi katika *Vita vya Mapenzi* kupitia “begi kubwa jekundu” alilokabidhiwa Suhail na Mzee Sufian. Begi hilo linaashiria damu, tamaa ya mali na maangamizi yanayoweza kutokea kutokana na tamaa hiyo. Ingawa begi hilo limejaa pesa nyingi, rangi yake nyekundu inamwonya msomaji kuwa utajiri huo umezungukwa na hatari na mateso. Begi lenye rangi nyekundu linajenga ishara ya damu na uhatarisho.

> *…. Suhail akijaribu kupingana na ukweli kwamba mzee Shamhurishi ameshakata roho, ghafla alipatwa na ujasiri akalifunga vizuri begi jekundu lenye pesa akalivaa mgongoni kisha akachukua begi dogo jeusi akalibeba mkononi na kuanza kutoka nje ya basi (uk18).*

Kitendo cha kukubali kulichukua “begi hilo kubwa jekundu” la kiajabu ni kujiingiza katika himaya ya udhalimu na utumwa wa maisha ambapo maisha yake yatakuwa yanadhibitiwa na kutawaliwa kwa njia fiche. Anakabiliwa na masharti yanayokuja kumtumbukiza katika usaliti wa kuhitilafiana na wanajamii, marafiki, familia yake pamoja na mpenzi wake Sharifa. Pesa aliyokabidhiwa katika begi jekundu inaonyesha sio tu tamaa ya pesa bali pia tamaa ya makuu mengine hali inayoishia kuashiria mabadiliko ya nafsi ya Suhail kama mtu binafsi, mabadiliko ya mtazamo wake wa ulimwengu, kuwapembeza wanafamilia na wanajamii waliowengi kwa sababu ya ushawishi wa mfumo wa uchumi anaojitambulisha nao kwa sasa na unaotawaliwa na pesa. Rangi nyekundu inamkumbusha msomaji kuwa ingawa pesa zimo kwa wingi lakini zinazungukwa na damu na hatari kubwa. Ishara ya wekundu inapaswa kumshitua msomaji kuwa kuna jambo la hatari ambalo limeizungukia hizo fedha nyingi;

> *Cha ajabu kila abiria akiliangalia lile begi dogo jeusi tu, na hakuna hata mmoja aliyejishugulisha kuangalia lile begi kubwa jekundu lilikuwa mgongoni ambalo ndilo hasa lenye pesa (uk 21).*

Abiria walio wengi ambao ni sawa na kundi kubwa la tabaka tawaliwa linashindwa kuuona mfuko mkubwa tena mwekundu, ila wanajishughulisha na kibegi kidogo cheusi. Hapa mwandishi anatupa taswira ya kiini macho ambacho wanajamii waliowengi wanashindwa kuiona rushwa kubwa na kujishughulisha na wizi mdogo mdogo au rushwa ndogo ndogo ambayo athari zake kwa jamii si kubwa. Rushwa kubwa hufanywa na viongozi wachache lakini athari yake kwa uchumi na michakato mingi ya kijamii ni kubwa mno. Kupiga vita rushwa ndogo, japo ni muhimu katika kukuza maadili, hakusaidii kuijenga jamii husika kwa njia chanya.

Aidha mabadiliko yangeweza kutokea iwapo wananchi au abiria waliowengi wangefanikiwa kuuona mzigo mkubwa wa rangi nyekundu wenye fedha nyingi mno ambazo mhusika Suhail angeshindwa kujieleza kwa waandishi wa habari, wananchi waliomzunguka au vyombo vya usalama na vile vya harakati za kupambana na wahujumu uchumi. Mfuko mkubwa mwekundu unaachiwa ukatelekeze sumu yake katika jamii. Suhail anakubali kuwa tayari kulitekeleza hilo baada ya kunasishwa katika mtego wa tamaa.

Ishara ya "begi jekundu" inajirudia katika *Mzimu wa Waufi* ambapo Masumbuko aliyekuwa akisafiri kutoka Dar es Salaam hadi Shinyanga kwenda kuwaona wazazi wake Mzee Kikoko na Mkewe Bi Kapemba aliye mke mkubwa na ili apate kuwahadithia mkasa wa utata wa ndoto yake, anaonekana akishuka katika basi akiwa na "Begi lake dogo jekundu" (uk.11). Wekundu huo huo bado unaendelea kuashiria hatari, maangamizo na ufu. Rangi nyekundu inaonekana tena katika kito cha pete ya "Khatam Budha" katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi* pale mhusika mkuu Suhail anapokabidhiwa na Mzee Sufian pete hiyo (uk 9).

Vilevile katika kutaharuki kwa inspekta Kenjah juu ya rangi ya pete anauliza swali lifuatalo kwa Suhail.

> *Nakumbuka kwenye maelezo Suhail uliandikisha kuwa una pete ya rangi ya kijani, sasa mbona hii ni nyekundu? (uk 9).*

Suhail hashituki kubadilikabadilika kwa pete hiyo, ila anashituka kwa vile "hiyo rangi nyekundu ikitokea tu ujue kuna hatari…hakujua ni hatari ipi inayotaka kutokea" (*Vita vya Mapenzi*: 210)". Kwa upande mwingine, Uidhir (2022) anaeleza kuwa rangi katika kazi za kifasihi huwa na uwezo wa kuathiri maamuzi ya wahusika na mwelekeo wa simulizi. Hoja hii inaonekana katika matumizi ya pete ya Khatam Budha ambayo hubadilika rangi kulingana na mazingira ya hatari au uponyaji. Kubadilika kwa rangi hizo kunaonyesha mabadiliko ya nafsi ya wahusika na migogoro ya ndani wanayopitia. Mabadiliko ya pete kuwa nyekundu ni ishara ya vita, damu na maafa. Wakati akiwa katika mazungumzo ya kutubu mbele ya wanafamilia yake, Suhail anaona pete ikibadilika rangi.

> *Akiwa katikati ya simulizi yake, mara pete yake ikabadili rangi na kuwa nyekundu. Ishara ya hatari! (uk 274).*

Utabiri huo ulithibitishwa na taarifa za Shekhia kuwa baba yake Mzee Sufian anauawa. Hivyo anaomba msaada kwa Suhail aende kumuokoa baba mkwe wake. Waliokuwa na pete katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi* ni Suhail na Shekhia. Shekhia anaitumia pete hiyo katika kumdhuru mke mwenzie Sharifa kwa ugonjwa wa kiharusi pia anaitumia pete hiyohiyo katika kumponyesha kwa kuibadilishabadilisha rangi kuwa ya kijani.

Rangi ya kijani inachukua dhima ya uponyaji badala ya rangi nyekundu inayoashiria hatari na vita. Aidha, Nemitz (2019) anasema kuwa rangi zina uwezo wa kubeba kumbukumbu za kitamaduni na kihisia katika jamii. Nemitz anaeleza kuwa nyekundu ni rangi ya nguvu, damu na tahadhari, huku kijani ikiwa ni rangi ya uzima, uponyaji na matumaini. Hoja hii inathibitishwa katika *Vita vya Mapenzi* pale Shekhia anapotumia miale ya kijani kutoka kwenye pete kumponya Sharifa aliyekuwa ameugua kwa nguvu za kichawi. Rangi ya kijani hapa inachukua nafasi ya nuru na tiba dhidi ya madhara ya nguvu za giza zilizowakilishwa na nyekundu.

Rangi nyingine iliyotumikishwa kwa mapana katika riwaya za Maundu Mwingizi, ni rangi nyeusi. Mara nyingi rangi nyeusi ni kielelezo cha ghubiko, utata, kiza au usiku. Huweza vilevile kumaainisha ubaya au maafa (Street 2017). Katika *Tanzia* chungu cheusi na kibuyu jeusi vinatumika katika kuwadhuru watu kiuchawi;

> *Wachawi wakalisogelea kaburi la hayati bwana Mtandi na kuanza kubinuka tena mahepe yao. Dakika chache tu Binti Sambayu akakipiga kwa nguvu chungu cheusi juu ya kaburi lile ba papohapo kaburi likapasuka na kuachia kijinjia chembamba (uk 61)*

Weusi wa chungu ni ishara ya ubaya, ulozi na vita. Kwa upande mwingine kibuyu kidogo alichokuwa nacho Bi Sambayu, nacho kinaelezewa na mtunzi kuwa kimehifadhiwa katika kapu lenye rangi ya kaki iliyogeuka na kuwa nyeusi kwa uchafu:

> *...kisha akaingiza mkono kwenye kikapu chake cha rangi ya kaki kilichoathiriwa na uchafu mpaka kikaonekana ni cheusi,*

*akakiweka kile kibuyu na kisha akatoa kitu kama mkufu hivi uliosukwa kwa ukindu, akamvisha binti Sambayu shingoni (uk 80).*

Unasibishaji wa uchafu na weusi ni taswira inayogonga vichwani mwa wasomaji. Mtunzi anaoanisha uchafu na weusi katika muktadha wa ulozi, ufufuaji na vifo. Haya ni mambo ambayo kwa usemi mwingine yanaashiria kudumaa kwa mawazo na maono ya watu katika jamii au makundi fulani ya jamii, ndio sababu ya kukwama kimaendeleo. Kwa pamoja tunaona mlandano wa rangi mbalimbali za njano, nyekundu na nyeusi katika pete ya Khatam Budha katika riwaya ya *Vita vya Mapenzi*, na kwa upande mwingine kibuyu cha uganguzi cha Babu Gao katika riwaya ya *Tanzia* kilichovikwa "shanga za rangi za njano, nyekundu na nyeusi (uk 28)." Tafsiri ya uchangamano wa rangi inahusiana na kazi na dhima ya pete katika *Vita vya Mapenzi* na kibuyu katika *Tanzia*. Dhima za kuponya na kudhuru kwa pamoja. Ikiwa ni rangi nyekundu pekee basi inakuwa ni dhima ya kuuwa na kuangamiza, ikiwa ni njano ni dhima ya maisha ya kawaida na tiba zake, na ikiwa ni nyeusi pekee ni dhima ya kuchawia na kuangamiza kiulozi kama ilivyo chungu cheusi cha wachawi wa Kibondo.

Kwa upande wa rangi nyeupe tumeiona sana katika mavazi yenye kuashiria ucha Mungu, furaha na utakatifu kama asemavyo Purev (2015) anaeleza kuwa katika jamii nyingi rangi nyeupe huhusishwa na utakaso, maadili mema na hali ya kiroho, ingawa katika baadhi ya tamaduni huweza kuhusishwa na maombolezo. Wakati wa harusi ya Suhail na Shekhia walikuwepo watu tisa waliovaa mavazi myeupe,

*Likikuwa ni kundi la watu kama tisa hivi, wakiwa wamevaa kanzu nyeupe huku wamejitanda vilemba vya rangi ya kijani wote kwa pamoja. Walikuwa ni watu wenye asili ya kiasia (uk 62).*

Rangi nyeupe na ya kijani zinaashiria upendo, amani, furaha na utakatifu. Anapoivaa kanzu "nyeupe pee" (uk. 245), Ustadh Hussein Chaullah alionekana pia akiwa na "tasbihi" na saa ya rangi ya almasi. Hali ya weupe pee ni ishara ya kuutafuta utakatifu na usafi wa mwili na roho. Mavazi meupe hupendelewa kuvaliwa na viongozi wa dini walio "wachamungu". Lakini pia katika mazingira mengine rangi nyeupe inaasharia uponyaji. Yalipoletwa maziwa, Ustadh Chaullah alibaini siri ya tiba ya maziwa ilivyo (*Vita vya Mapenzi* uk. 278). Anasema kwamba, "kuna siri kubwa ndani ya maziwa, siri ya kiafya na kitabibu."

Msomaji anaposoma kazi za riwaya za Mwingizi rangi inayotawala kwa wingi kupitia vito na damu za makafara ni rangi nyekundu. Rangi nyekundu na nyeusi ni rangi za ushetani, nguvu za giza, ushenzi na usaliaji nyuma kimaendeleo ilhali rangi nyeupe ni rangi ya afya, maisha, uangavu, uokovu na umalaika. Ushetani unatawala kazi zake na kiashirio kinachompelekea kiongozi mmoja wa serikali kuwafokea viongozi wengine:

*Shut up, haya niambie nani msafi humu kati yenu? Kila mmoja ana yake aliyoyafanya kwa njia yake katika kujihakikishia analinda ugali wake…nani asiyetaka madaraka humu? Nani asiyetaka mali humu? (uk. 286).*

Aidha weusi mkubwa na kiza kilichotanda kilikuwa kinawekwa na viongozi wasaliti chini ya mtandao wa *Black Scorpion* (*Vita vya Mapenzi*: 286). Maana ya "Black" ni weusi. Walikuwa wanatia kiwingu wanajamii ili kuendelea na kupiga hatua kimaisha na kiustawi kwa kuwahujumu kiuchumi. Kiza kingine kilikuwa kinawekwa na himaya ya *Khatam Budha*. Nao walibidi waangamizwe kwa damu ili weupe utawale na uondoe kiza. Kiza na weupe ni nguvu mbili ambazo haziwezi kuchanganyika. Nguvu ya weupe inapambana na nguvu ya weusi. Wahusika weupe wanawakilishwa na Ustadh Chaulla, ambaye naye anafanya kazi ya usalama wa taifa kwa siri, mwanadada Lillian Ufoo naye anawakilisha weupe, na uzuri lakini akiwa kwa siri na yeye ni mwanausalama.

Hii ikiwa ni siri yake. Naye Mirzoeff (2021) anasema kuwa matumizi ya rangi katika fasihi na sanaa huonyesha mgongano wa nguvu katika jamii. Katika riwaya za Mwingizi, mgongano kati ya rangi nyeupe na nyeusi unaashiria mapambano kati ya wema na uovu. Weusi unaonekana kupitia mtandao wa "Black Scorpion" unaohusishwa na viongozi wasaliti wanaotumia giza kuhujumu jamii kiuchumi, huku weupe ukiwakilishwa na wahusika wanaotafuta haki na ukombozi wa jamii.

Rangi nyekundu licha ya fahiwa nyingi za uashiriaji, ni rangi ya damu. Mateso na vifo vinavyotokana na umwagikaji damu vinatapakaa katika riwaya za Mwingizi. Suhail anapigwa na Komandoo Takadir na

kutapakaa damu akiwa kizuizini. Amanda anachukuliwa na kimbunga na kurudishwa chini akiwa maiti. Msigwa anakufa akiwa na majeraha ya risasi yaliyomtoa damu nyingi, Mzee Sufian na Komandoo Takadir wanaangamizwa kwa moto mwekundu na wakiwa wameloa damu. Ujumbe tunaoupata ni kuwa tamaa ya pesa na mali inapelekea kutoweka kwa utu, ubinadamu, uungwana na ustahili na badala yake kuotesha kutokwa damu nyekundu ambayo hatima yake ni kuangamia. Damu zinazowatoka wahusika ndani ya *Vita vya Mapenzi* ni malipo ya matendo ya tamaa, uongo na usaliti. Zana ya pete inawakilisha hali za wanajamii, yaweza kupewa kafara la damu kwa mwenye kutaka kuitumia kwa mauaji na maangamizi au kwa kafara la maziwa kwa mwenye kutaka kuitumia kwa ajili ya utakaso, kutafuta haki na kujirudi. Kito cha pete hakina rangi maalumu bali inategemea nia ya mvaaji.

**Mazingira na Uasilia kama Ishara na Uashiriaji**

Kwa mujibu wa Zapf (2016), mazingira katika fasihi hutumika kama mfumo wa kiutamaduni unaoonyesha migogoro ya jamii na mabadiliko ya maisha ya binadamu. Zapf anaeleza kuwa vipengele vya mazingira kama dhoruba, upepo na giza si maelezo ya hali ya hewa pekee, bali ni alama za migogoro ya ndani ya jamii. Ishara na uashiriaji katika mazingira ya uasilia katika riwaya za Mwingizi zimeonekana katika ishara zinazohusianishwa na hali ya hewa kama ukungu, upepo, mbalamwezi, upinde, vimbunga, mvua, kiza na nuru. Ni sehemu muhimu katika kuashiria tanzia na maangamizo ya baadhi ya wahusika wakuu katika riwaya teule za Mwingizi. Sehemu kubwa ya ishara hizi huonekana katika kipengele cha mandhari.

Kama zilivyo ishara mbalimbali, kuna kubaini hali ya ukweli na ile ya kuwakilisha aina fulani ya maana ya ziada. Ishara hizo hufanikiwa iwapo mwandishi atazitumia kufikisha pande zote mbili za maana bila ya kuwashurutisha wasomaji kubaini maana hizo. Tunapenda kuthibitisha katika sehemu hii kuwa Mwingizi amefaulu kufikisha kwa wasomaji wake aina zote mbili za maana zinazokuwa ni kielelezo cha ujumbe anaoukusudia. Mwandishi anawachorea wasomaji wake katika *Vita vya Mapenzi* (uk. 276) ishara ya upepo usio wa kawaida:

> *Wakati hayo yakiendelea ghafla hali ikabadilika ukasikika upepo mkali ukivuma huko nje, vumbi la haja likitimka. Milango ikijibamiza. Upepo ulikuwa mkali sana kiasi cha kufanya uingie mpaka barazani…. ilikuwa ni kimbunga kikubwa kilichofuatiwa na harufu kali ya marashi iliyotanda takribani kwa dakika tano! (uk. 276).*

Upepo huu unaashiria mapambano ya majini wawili katika viwiliwili vya Mzee Sufian bin Shahurish na Komando Takadir Alharab. Aidha, Žižek (2024) anasema kuwa majanga na vurugu katika kazi za kifasihi mara nyingi huwa ishara ya mifumo fiche ya hofu na migogoro ya kijamii. Katika riwaya hii Vita *vya Mapenzi*, upepo mkali na harufu ya marashi inayofuatia mapambano ya majini inaonyesha uwepo wa nguvu zisizoonekana zinazotawala maisha ya wahusika. Hivyo mazingira yanakuwa sehemu ya kujenga ulimwengu wa kifalsafa na kiimani katika simulizi.

Ishara ya giza ni ishara bia yaani ni ishara ambazo hujulikana na jamii mbalimbali duniani kote. Hivyo basi ishara ya giza katika kazi za fasihi hutumiwa kusimamia hali ya kutojua, hali ya kughubikwa, hali ya ukosefu wa ufahamu. Kwa upande mwingine Lawrence (2001: 2) anasema giza ni ishara ya hofu, hatari na hali ya kukosa matumaini. Kwa upande mwingine giza huwa ishara ya uovu, hatari au ujinga (Frye na wenzake 1985: 453). Naye Oppermann (2018) anaeleza kuwa mazingira katika fasihi hujenga "mawasiliano ya kiishara" kati ya binadamu na ulimwengu unaomzunguka.

Kwa mujibu wake, vipengele vya asili vinaweza kuakisi hali za kiroho, hofu na mifumo ya utawala katika jamii. Hoja hii inajitokeza katika *Mzimu wa Waufi* ambapo giza linaloletwa na Hunudu linaashiria ukandamizaji wa fikra na kupotea kwa elimu ya kujitambua. Mwingizi analitumia giza kama ishara ya jamii iliyofunikwa na mifumo kandamizi inayowafanya watu washindwe kutambua haki zao. Katika riwaya hii ya kimajaribio ishara ya giza imechimuza maudhui mbalimbali. Ishara hizi za giza zimetumika tena katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi* katika uk. 150 na uk. 213 ambapo mtunzi anaonyesha ishara ya giza kama elimu ya kutojitambua.

Kwa upande mwingine, Garrard (2019) anasisitiza kuwa fasihi ya kisasa hutumia majanga ya mazingira kama sitiari ya migogoro ya kisiasa na kijamii. Kwa mtazamo huu, vimbunga na dhoruba katika riwaya za Mwingizi vinaweza kutafsiriwa kama ishara ya mapambano ya nguvu ndani ya jamii. Kwa mfano, kimbunga kilichoishambulia teksi ya Mzee Mtandi katika *Tanzia*

hakikuwa hali ya hewa ya kawaida, bali ni ishara ya vita vya nguvu za kichawi na mauti inayomkabili mgonjwa. Hivyo mazingira yanatumika kuonyesha hali ya sintofahamu na hatari inayonyemelea jamii. Katika riwaya ya *Tanzia,* mtunzi Mwingizi anatumia ishara za upepo mkali, ukiambatana na usiku wa kiza kinene;

> *Upepo ule mkali uliendelea kuvuma mithili ya kimbunga huku baridi kali ikiwa imeshtadi kwelikweli (uk 1).*

Upepo huo haukuwa wa kawaida kwani kipindi hicho kilikuwa ni cha kiangazi katika mji huo wa Kibondo. Siri kubwa ya mabadiliko ya hali ya hewa ya kiasi cha kuogofya ilitokana na imani kwamba, Kikongwe Bi Masonganya aliyekuwa mchawi maarufu alikuwa anakata roho. Ndugu, watoto, wajukuu na vitukuu vyake walimfanyia dawa ya kumtoa roho ili asimrithishe mtu uchawi wake. Kwa hivyo hapa mtunzi analizungumzia suala la kuvunja na kutupa mifumo shenzi ya imani zinazokwamisha watu katika maendeleo yao.

Katika riwaya ya *Tanzia* mwandishi Mwingizi anawachorea wasomaji wake taswira ya usiku wenye giza kuu na dhoruba za mvua kali katika mji wa Kibondo ikiashiria tukio la kufariki mtu mkubwa, Bi Masonganya binti Kalukalange ambaye inasemekana kuwa alikuwa mchawi aliyebobea katika taaluma hiyo. Kunyesha kwa mvua kubwa na giza totoro ni ishara aliyoitumia mwandishi kuwapa wasomaji wake picha ya huzuni na maafa yanayoikabili jamii hiyo. Ni alama inayofasirika na wanajamii wa Kibondo kuwa ni mawasiliano ya nguvu za ujaala. Kimbunga kikali kiliishambulia teksi waliokuwemo Mzee Mtandi na nduguze mama Kaguba na Kungurume wakati wa kumpeleka kwa mganga aitwaye Babu Gao;

> *Walipofika katika moja ya mapori kadhaa ambapo ilikuwa wakilimaliza tu pori lile wangewasili nyumbani kwa Babu Gao, ndipo kilipoibuka kimbunga kikali kilichoishambulia ile teksi mpaka ikapoteza uelekeo na kuzima (uk 37).*

Kimbunga hicho si cha kawaida bali ni cha mashambulizi ya akina Kaguba na Binti Sambayu na wachawi wengine. Ishara ya kimbunga hainasibishwi na hali ya hewa bali hutafsirika kama dalili ya vita na kifo kinachomnyemelea mgonjwa.

Aidha kwa upande mwingine giza limetumika kama ishara ya kukosa matumaini kwani mataifa mengi ya Afrika wananchi wake wamekata tamaa na hawana matumaini kwa sababu wamejawa na hofu kubwa juu ya viongozi wao. Kwani wamekuwa na viongozi ambao hawana msaada kwao na pindi wanapotaka kuandamana kwa ajili ya kupata haki zao wamekuwa wakinyamazishwa kwa wengine kuuliwa na wengi kutishiwa maisha. Kwa hiyo hali imezidi kuwa tete na kuendelea kukosa matumaini kabisa na huona heri ya jana yao kuliko leo yao.

Kwa upande mwingine mtunzi ametumia giza katika tukio hili la kina Hunudu kiishara kuashiria hali ya wanataaluma kutojua umuhimu wa taaluma wanazokuwa nazo. Wanashindwa kutekeleza majukumu yao kwa jamii na taifa, walichobaki nacho ni vyeti na viwango vya elimu visivyo na tija kwani muda wote huonekana kutukuza mambo ya kigeni na kudharau ya kwao. Katika uk. 213 katika riwaya ya *Mzimu wa Waufi* mtunzi anaonyesha Hunudu akileta giza kubwa walipokuwa wanamzika Nyamizi halafu mbele ya lile giza kuna mwanga.

Hii inaonyesha wazi kabisa wasomi wamepewa elimu ili waweze kujitambua lakini bado wanapenda kukaa gizani wakati mbele yao kuna mwanga. Kwa mfano mzuri hakuna nchi ambayo imeendelea dunia pasipo kutumia lugha ya kwao lakini wasomi wengi ndio wamekuwa msitari wa mbele katika kutetea lugha zingine na kuzipamba kitu ambacho kinapelekea hata maendeleo kuzorota katika nchi zao. Hii ni kwa sababu hata lugha nayo ina mchango mkubwa katika ukuzaji wa maendeleo kwa hiyo elimu tulioipata bado haijaweza kutufikisha kwenye mwanga.

Kwa upande mwingine mwandishi anaonyesha kuwa Waswezi katika riwaya *Mzimu wa Waufi* pia hutumia mwanga au nuru kama ishara ya elimu ya kujitambua, kwani Mwangaza huashiria ukweli, ufahamu, usalama au wema (Hall 1996: 91), kwa mfano katika uk. 214 na 215 tunaona Hunudu amewavamia Waswezi makaburini katika mazishi ya Nyamizi aliyeuawa na Hunudu. Kijana huyo katili alikuja kwa njia ya giza. Ingawa wakati wa mapambano yakiendelea ndani ya giza lililoletwa na Hunudu, wazee wa Kiswezi waliendelea kupambana kurudisha mwanga. Mwandishi anasema:

> *…wakafanikiwa kwani ndani ya muda ule wa mapambano mwanga ukarudi na*

*kila mmoja sasa akamwona Hunudu vizuri lakini inaonekana kuwa Hunudu hakutaka mwanga kabisa katika kutimiza mauaji aliyoyakusudia… (uk. 215).*

Kwa mujibu wa Huggan na Tiffin (2021), mazingira katika fasihi ya Kiafrika hutumiwa kufichua migogoro ya kiutamaduni na kiitikadi. Wataalamu hawa wanaona kuwa matumizi ya nuru na giza huwa mbinu ya kuonyesha mgongano kati ya maarifa na ujinga. Katika riwaya hii ya *Mzimu wa Waufi*, nuru inayorejeshwa na Waswezi wakati wa mapambano dhidi ya Hunudu inaashiria kurejea kwa ukweli, haki na elimu ya kujitambua. Hii inaonyesha kuwa mwanga ni alama ya ukombozi wa jamii dhidi ya nguvu za ukandamizaji.

Kwa mantiki hii ishara ya giza ni ishara ya waovu, na pia ishara ya kuwatoa watu ufahamu. Lakini kwa Waswezi ishara ya mwanga ni elimu ya utambuzi na uwazi pia. Ndio maana baada ya kukandamizwa kwa muda mrefu na Waufi, wananchi wanapata elimu ya kujitambua wanapambana na serikali iliyopo mamlakani na wanafanikiwa kuwaondoa Waufi. Hatimaye, Nabukonde (2012) anaeleza kuwa fasihi ya Kiafrika ya kisasa imeendelea kutumia mazingira kama lugha ya kisiasa na kijamii inayowawezesha waandishi kuikosoa jamii bila kutumia lugha ya moja kwa moja. Katika riwaya za Mwingizi, ishara za giza, vimbunga na nuru zinawakilisha ukandamizaji, mapambano na ukombozi wa jamii ya Kiafrika inayotafuta mwanga wa maendeleo na utambuzi.

## HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

**Hitimisho:** Makala hii inaonyesha kuwa uashiriaji katika riwaya teule za Maundu Mwingizi si mbinu ya kisanaa ya kupamba lugha pekee, bali ni nyenzo muhimu ya kujenga maana, kuwasilisha fikra za mwandishi na kufichua changamoto za kijamii kwa kina. Uchanganuzi uliofanywa umebainisha kuwa matumizi ya ishara mbalimbali yanajenga uhusiano wa karibu kati ya tajriba za kijamii, mitazamo ya kiutamaduni na mawanda ya kifalsafa yanayoibuliwa katika riwaya husika.

Hivyo, utafiti huu umeongeza uelewa kuhusu nafasi ya uashiriaji kama mkabala wa kifasihi unaowezesha kufasiri matini za Kiswahili kwa mtazamo mpana unaozingatia muktadha wa jamii na utamaduni. Aidha, utafiti huu unatoa mchango katika taaluma ya fasihi ya Kiswahili kwa kupanua maarifa kuhusu matumizi ya uashiriaji katika riwaya za Maundu Mwingizi, eneo ambalo halijapewa uzito wa kutosha katika tafiti zilizotangulia.

**Mapendekezo:** Kwa msingi huo, inapendekezwa tafiti zijazo zichunguze kwa kina namna uashiriaji unavyochangia ujenzi wa ploti, wahusika, mandhari na mtazamo wa mtunzi katika riwaya za Kiswahili. Vilevile, tafiti zinaweza kuelekezwa katika uchambuzi wa uashiriaji wa majina, pamoja na kulinganisha matumizi ya uashiriaji katika kazi za Maundu Mwingizi na waandishi wengine wa riwaya za Kiswahili ili kupanua zaidi upeo wa maarifa katika eneo hili.

## REFERENCES


Abrams, M. H. (1971). *A glossary of literary terms*. Holt, Rinehart & Winston.

BAKITA. (2023). *Kamusi kuu ya Kiswahili* (Toleo la 3). Longhorn Publishers.

Baudrillard, J. (1998). *The consumer society: Myths and structures*. Sage Publications. (Original work published 1970)

Berlin, B., & Kay, P. (1969). *Basic color terms: Their universality and evolution*. University of California Press.

Birkerts, S. (1993). Symbolism. In *Literature: The evolving world*. Allyn & Bacon.

Caminero-Santangelo, B. (2023). *Different shades of green: African literature, environmental justice, and political ecology*. Routledge.

Chandler, D. (2007). *Semiotics: The basics* (2nd ed.). Routledge.

Cirlot, J. E. (1962). *A dictionary of symbols*. Routledge & Kegan Paul.

Clark, T. (2020). *The value of ecocriticism*. Cambridge University Press.

DiYanni, R. (1998). *Literature: Reading fiction, poetry and essay* (4th ed.). McGraw-Hill.

Eagleton, T. (1983). *Literary theory: An introduction*. Blackwell.

Frye, N., Baker, S., & Perkins, G. B. (1985). *The Harper handbook to literature*. Longman.

Garrard, G. (2019). *Ecocriticism* (3rd ed.). Routledge.

Han, B.-C. (2017). *Psychopolitics: Neoliberalism and new technologies of power*. Verso Books.
Harari, Y. N. (2015). *Sapiens: A brief history of humankind*. Vintage Books. (Original work published 2011)
Huggan, G., & Tiffin, H. (2021). *Postcolonial ecocriticism: Literature, animals, environment*. Routledge.
Kihore, F. M. (1999). *Semantiki: Nadharia na misingi ya Kiswahili*. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
Lawrence, D. H. (2001). *Apocalypse and the writings on revelation*. Cambridge University Press.
Leeuwen, T. van. (2016). *Multimodality and identity*. Routledge.
Maguo, O. M., & Alhabib, E. A. (2020). Mtindo na wahusika katika diwani za *Dhifa* na *Wasakatonge*. *MULIKA, 39*, 50–65.
Malugu, A. (2016). Nafasi ya fasihi katika kusawiri suala la dini. *Kiswahili, 79*, 66–77. https://journals.udsm.ac.tz/index.php/kiswahili/article/view/743
Maundu Mwingizi. (2012). *Vita vya mapenzi*. Gama Printers.
Maundu Mwingizi. (2013). *Mzimu wa Waufi*. Gama Printers.
Maundu Mwingizi. (2015). *Tanzia*. Gama Printers.
Mazrui, A. A. (1986). *The political sociology of the English language: An African perspective*. Mouton de Gruyter.
Mbembe, A. (2019). *Necropolitics*. Duke University Press.
Mbiti, J. (2022). *African religions and philosophy* (Updated ed.). East African Educational Publishers.
Meyer, M. (2002). *The Bedford introduction to literature*. Bedford/St. Martin's.
Mohammed, M. A. (2001). *Modern Swahili grammar*. East African Educational Publishers.
Möhlig, W. (1981). *Colour terms in African languages*. Dietrich Reimer Verlag.
Nabukonde, L. L. (2012). *Symbolism in Ugandan poetry* (Unpublished doctoral dissertation). University of Nairobi.
Neimanis, A. (2022). *Bodies of water: Posthuman feminist phenomenology*. Bloomsbury Academic.
Ngũgĩ wa Thiong'o. (1986). *Decolonising the mind*. Heinemann.
Ngũgĩ wa Thiong'o. (2021). *Decolonising the mind* (Rev. ed.). East African Educational Publishers.
Oppermann, S. (2018). *Environmental humanities and new materialisms: The matter of narrative*. Rowman & Littlefield.
Perrine, L. (2014). *Literature: Structure, sound, sense*. Wadsworth.
Purev, T. (2015). A comparative study on color metaphor in Mongolian and English. *Mongolian Journal of Foreign Languages and Cultures*. https://doi.org/10.22353/MJFLC2015120
Riffaterre, M. (1978). *Semiotics of poetry*. Indiana University Press.
Robert, S. (1951). *Kusadikika*. Nelson.
Saussure, F. de. (1916). *Course in general linguistics*. McGraw-Hill.
Snowden, R. (2006). *Freud: The key ideas*. Hodder Education.
Street, S. (2017). *Colour films in Britain: The negotiation of innovation*. Palgrave Macmillan.
Turner, V. (1967). *The forest of symbols*. Cornell University Press.
Uidhir, C. M. (2022). *Art and narrative meaning*. Routledge.
Wamitila, K. (2002). *Nadharia ya fasihi na uhakiki*. Focus Publishers.
Wa Mutiso, K. (1996). *Archetypal motifs in Swahili Islamic poetry: Kasida ya Burudai* (Doctoral dissertation). University of Nairobi.
Walter Rodney. (2014). *How Europe underdeveloped Africa*. East African Educational Publishers.
Zapf, H. (2016). *Literature as cultural ecology: Sustainable texts*. Bloomsbury Academic.
Žižek, S. (2024). *Violence and the environment in contemporary thought*. Verso Books.